



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MJINI MAKAMBAKO
(Mawasiliano yote yafanywe kwa Mkurugenzi wa Mji)



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na: MTC/I.20/2.VOL I/68

01/10/2024

TANGAZO

KWA UMMA HALMASHAURI YA MJINI MAKAMBAKO KUHUSU KUFUNGULIWA KWA UTOAJI WA MIKOPO KWA VIKUNDI VYA WANAWAKE, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU.

(Limetolewa kwa kuzingatia Kanuni ya 7 (1) ya utoaji na usimamizi wa mikopo ya vikundi vya Wanawake, Vijana na watu wenye ulemavu za mwaka 2024.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Makambako anatangaza kufunguliwa kwa mikopo ya vikundi vya Wanawake, Vijana na watu wenye ulemavu na uwepo wa fedha kwa ajili ya kuvikopesha vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, ambapo jumla ya **Shilingi 559,770,149.58** zimetengwa katika robo ya 1 ya mwaka wa fedha. 2024/2025 kwa ajili ya kuvikopesha vikundi vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Hivyo, Vikundi vyenye sifa vinakaribishwa kuleta maombi kwa njia ya mfumo wa usimamizi na utoaji wa Mikopo (wezesha portal)

Maombi yatapokelewa katika **Ofisi za Mtendaji Kata** zilizopo katika maeneo yenu.

Vikundi vinavyotakiwa kuomba mikopo vinapaswa kuwa na sifa zifuatazo: -

- i. Kikundi cha wanawake, vijana na watu wenyewe ulemavu kilichotambuliwa na kupewa cheti cha utambuzi na Halmashauri kwa njia ya mfumo wa kieletroniki. (Wezesha portal)
- ii. Kikundi kiwe kinachojishughulisha na shughuli za ujasiriamali mdogo au wa kati au kikundi kinachotarajia kuanzisha shughuli za ujasiriamali,
- iii. Kikundi cha Wanawake na Vijana kiwe na idadi ya wanakikundi kuanzia watano (5) na kuendelea na kikundi cha watu wenyewe ulemavu kiwe na wanakikundi wasiopungua wawili (2). Pia kwa kuzingatia kanuni ya 6 a(1) Mtu mwenye ulemavu anaweza kuwa na sifa ya kupata mkopo kama kikundi cha watu wenyewe ulemavu endapo Timu ya Menejimenti ya Halmashauri itajiridhisha kuwa amekosa mtu mwingine mwenye ulemavu wa kuungana naye katika eneo lake. Aidha sifa zingine zitafanana na sifa za vikundi vingine,
- iv. Kikundi kiwe na akaunti ya benki iliyofunguliwa kwa jina la kikundi kwa ajili ya matumizi ya shughuli za kiujasiriamali za Kikundi.
- v. Wanakikundi lazima wawe ni raia wa Tanzania wasio na **Ajira Rasmi**, wenyewe akili timamu na wenyewe umri wa kuanzia miaka 18 na kuendelea. Aidha, kikundi cha vijana kitapaswa kuwa na wanakikundi wenyewe umri kuanzia miaka **18 hadi 45**.


Maombi yote yatumwe kupitia mfumo wa kielekroniki (**tembelea tovuti: mikopohalmashauri.tamisemi.go.tz**) ili kutambuliwa na kuomba mkopo au wasiliana na Afisa Maendeleo ya Jamii wa Kata husika au Mtendaji wa Kata husika.

Kikundi kinachoomba mkopo kinapaswa kuwa na viambatisho vifuatavyo;

- i. Barua ya kikundi ya kuomba mkopo iliyopitishwa na Afisa mtendaji wa kijiji/mtaa kwa kuandika jina lake, saini na kugonga mhuri wa serikali ya Kijiji/Mtaa,
- ii. Muhtasari wa kikundi wa kuomba mkopo
- iii. Andiko rahisi la mradi unaoombewa mkopo kwa kuzingatia fomu iliyo ndani ya mfumo wa kieletroniki
- iv. Taarifa ya akaunti ya benki yenye jina la kikundi au Jina la mtu mwenye ulemavu mmoja aliyekosa wenzake wa kuungana nao

Mwisho wa kuwasilisha maombi ni tarehe **22/10/2024**

Tangazo hili limetolewa na: -


Kenneth K Haule
Mkurugenzi

HALMASHAURI YA MJI MAKAMBAKO

***MKURUGENZI
HALMASHAURI YA MJI
MAKAMBAKO***